## VIFUPISHO VYA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| CBOs | – | Community Based Organizations |
| CSOs | - | Civil Society Organizations |
| CUF | - | Civil United Front |
| CHADEMA | - | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| DALDO | - | District Agriculture and Livestock Development Officer |
| DCDO | - | District Community Development Officer |
| DCO | - | District Cooperative Officer |
| DE | - | District Engineer |
| DED | - | District Executive Director |
| DEO (M) | - | District Education Officer (Primary) |
| DEO (S) | - | District Education Officer (Secondary) |
| DFsO | - | District Fisheries Officer |
| DIA | - | District Internal Auditor |
| DLaDO | - | District Land Development Officer |
| DMO | - | District Medical Officer |
| DNRO | - | District Natural Resources Officer |
| DPLO | - | District Planning Officer |
| DT | - | District Treasurer |
| DVO | - | District Veterinary Officer |
| DWE | - | District Water Engineer |
| FsO | - | Fisheries Officer |
| HBF | - | Health Basket Fund |
| HIV/AIDS | - | Human Immune deficiency Virus/Acquired Immune Deficiency Syndrome |
| IEC | - | Information Education Communication |
| LAAC | - | Local Authority Accounts Committee |
| LGAs | - | Local Government Authorities |
| LGCDG | - | Local Government Capital Development Grant |
| LO | - | Legal Officer |
| MKURABITA | – | Mpango wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge Tanzania |
| MM | - | Mpango Mkakati |
| MTEF | - | Medium Term Expenditure Framework |
| NAO | - | National Audit Office |
| NEC | - | National Electral Commission |
| NGOs | - | Non Governmental Organizations |
| PMO-RALG | - | Prime Minister’s Regional Administration and Local Government |
| PMU | - | Procurement Management Unit |
| PPA | - | Public Procurement Act |
| PPR | - | Public Procurement Regulation |
| SACCO | - | Saving and Credit Cooperative Societies |
| TACAIDS | - | Tanzania Commission for AIDS |
| TANROADs | - | Tanzania Roads Agency |

| | | |
|---|---|---|
| TLP | – | Tanzania Labour Party |
| TTCL | - | Tanzania Telecommunication Coperation Limited |
| TASAF III | - | Tanzania Social Action Fund III |
| VVU/UKIMWI | – | Virusi vya UKIMWI/ Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| VEOs | - | Village Executive Officers |
| WDC | - | Ward Development Committee |

# MPANGO MKAKATI WA HALMASHAURI YA MISSENYI

# (2020/2021 - 2024/2025)

## SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 MAELEZO MAFUPI YA MPANGO MKAKATI

Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi umezingatia mahitaji yote yaliyopo katika Taasisi kwa kuangalia shughuli na mahitaji ya kila Idara na Vitengo. Mpango unatekelezwa kwa miaka mitano kuanzia 2020/2021 hadi 2024/2025 ikiwa umeuhishwa kutoka mpango ulioisha muda wake wa mwaka 2018 – 2022.Mpango huu unaainisha kwa undani vipengele vya mpango mkakati makini kulingana na mwongozo wa uandaaji wa mpango mkakati. Pia unaelezea sisi kama Taasisi tupoje kwa sasa,yapi ni malengo tunayopanga kufikia na jinsi gani tumejipanga katika kufikia malengo hayo. Mpango Mkakati unaonesha mazingira ya sasa ya kazi na historia ya Taasisi ambayo inatoa mwelekeo sahihi wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kulingana na sera zilizopo. Mpango huu ni matokeo ya ushirikiano mzuri uliopo baina ya Halmnashauri na Wadau wake muhimu. Mchakato mzima wa uandaaji wa Mpango huu ulihusisha kufanya uchambuzi wa hali halisi ya Wilaya na kuhitimishwa na masuala nyeti yanayohitaji kupewa kipaumbele katika Mpango kwa kutengenezea Dira, dhamira, miiko, malengo, shabaha na maeneo muhimu ya matokeo tarajiwa. Jukumu kubwa la Halmashauri ni kutoa huduma endelevu na zenye ubora wa juu za kijamii na kiuchumi kwa wananchi wake.

### 1.2 UANDAAJI WA MPANGO MKAKATI

Mpango Mkakati wa Halmashauri wa miaka mitano (2020 -2025) umeandaliwa kwa kufanya mapitio ya mpango mkakati uliopita wa mwaka (2018 -2022). Msukumo wa kuandaa Mpango huu ulitokana na sababu mbalimbali kama vile;

- Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020 – 2025)
- Mahitaji ya utoaji huduma kwa wananchi
- Mabadiliko ya Sera, Vipaumbele, Mipango ya Serikali

- Hali halisi ya kiuchumi ya Wananchi.
- Ukuaji na ushirikishwaji wa Sekta binafsi
- Umuhimu wa uwajibikaji wa Sekta ya Umma

Mpango huu ni shirikishi ambapo umejumuisha mipango ya maendeleo na mahitaji ya wadau mbalimbali wa maendeleo walioketi kupitia mikutano mbalimbali ya Vijiji, Kata, Baraza la Madiwani, Wadau wa maendeleo, Elimu na Afya ikiwa ni pamoja na Viongozi wa Serikali, Wawakilishi wa wananchi, Taasisi za dini na mashirika binafsi.

Kuwepo kwa Mpango Mkakati huu kutawezesha Halmashauri kutoa huduma bora kwa jamii, kuongeza kipato kwa kaya, kukuza uchumi na kupunguza umaskini, kuhakikisha ulinzi na usalama wa wananchi unaimarishwa ili kufikia malengo, Dhamira na Dira ya Halmashauri, Ilani ya uchaguzi ya Chama Tawala (2020 – 2025) na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

### 1.3 MALENGO YA MPANGO

Malengo ya Mpango huu ni kuhuisha malengo, mikakati na shabaha za Wilaya ili kuhakikisha mipango ya utatuzi wake inakizi kwa kila eneo. Mpango una lengo la kujumuisha jitihada, programu au miradi yote ya Halmashauri ili kuwa katika Mpango mmoja madhubuti wa utekelezaji.

Aidha, mpango huu una lengo la kuwafahamisha wadau wetu nini tumepanga kufanya, kutoa mwongozo utakaowaelekeza jinsi ya kushirikiana nao na pia kuonesha uwazi, uwajibikaji na majukumu kati ya menejimenti, watumishi, wateja na wadau wengine na kutengeneza vipaumbele vyenye ufanisi na uendelevu wakati wa ugawaji wa rasilimali

### 1.4 MPANGILIO WA MPANGO MKAKATI (KITABU)

Mpangilio wa Mpango huu umezingatia mwongozo wa kitaifa wa uandaaji wa Mpango Mkakati ambao unasisitiza kuwa na sura nne kama ifuatavyo;

**SURA YA KWANZA:** Sura hii inajumuisha utangulizi, maelezo mafupi kuhusu Halmashauri. Pia ina maelezo ya njia iliyotumika kuandaa Mpango. Sura inaenda Zaidi kwa kuelezea malengo ya mpango na mwisho mpangilio mzima wa Kitabu

**SURA YA PILI:** Inahusu mpango uliopita kwa kufafanua Uchambuzi wa hali halisi ya Wilaya ambapo maswali yanayohusu Taasisi yanapata majibu kutokana na takwimu za kiutafiti. Inaonesha taasisi ilipotoka, ilipo sasa na muelekeo wake na njia/hatua itakazotumia kupitia mikakati iliyojiwekea kwa kipindi kijacho yaani 2020 – 2025. Vipengele vya uchambuzi wa hali halisi ya Wilaya vilivyomo katika sura hii ni; Historia fupi, jukumu na wajibu wa kisheria, Dira na Dhima iliyopita, mapitio ya utekelezaji (Mafanikio, kutofanikiwa na nini kifanyike kwa kila malengo ya Mpango uliopita), matokeo ya utafiti wa utoaji huduma na tathmini ya ndani ya Taasisi, uchambuzi wa wadau, uchambuzi ndani na nje ya Taasisi, hatua/jitihada kuimarisha utendaji na masuala muhimu ya kuwekewa Mkakati.

**SURA YA TATU:** Inaelezea mpango unaokwenda kuhuishwa, ambapo inajumuisha vipengele vya Dira, Dhima, Miiko ya Taasisi, Malengo, Mikakati, Shabaha na viashiria muhimu vya upimaji wa matokeo

**SURA YA NNE:** Ni mfumo wa upimaji matokeo ambao unajumuisha mpango wa Ufuatiliaji na tathmini ambao umegawanyika katika maeneo yafuatayo; muundo na malengo, malengo ya kimaendeleo, wanufaika wa huduma za taasisi, uhusiano na mpango wa maendeleo wa miaka mitano awamu ya II, mnyororo wa matokeo, mpango wa kutoa taarifa na mwisho mpango una viambatisho ambavyo ni muundo wa Wilaya, fremu ya utoaji matokeo na fremu ya Mpango wa ufuatiliaji

## SURA YA PILI

### 2.0 UTANGULIZI

Wilaya ya Missenyi ni miongoni mwa Wilaya nane (8) za Mkoa wa Kagera.ilianzishwa tarehe 01 Julai, 2007 chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa No. 7 ya mwaka 1982, kupitia Tangazo la Serikali No.87 baada ya kugawanywa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba. Halmashauri ilianza kutekeleza majukumu yake ya kimamlaka kuanzia Julai, 2008. Jukumu kubwa la Halmashauri ni kutoa huduma endelevu na zenye ubora wa juu za kijamii na kiuchumi kwa wananchi wake.

## 2.1UCHAMBUZI WA HALI HALISI YA WILAYA

Uchambuzi wa hali halisi unatumika kuonesha mapungufu muhimu na sababu zake ndani au nje ya Taasisi. Hii ni kupitia hatua ya utambuzi wa tatizo, dhumuni likiwa ni kutambua mapungufu ya utoaji wa huduma katika Halmashauri, sababu za mapungufu hayo za ndani na nje ya Taasisi. Hatua hii inahusisha kuchambua matokeo ya utekelezaji wa utoaji wa huduma kwa kila Idara, Kata na Vijiji ambapo mapungufu ya utoaji huduma yananyumbulishwa kwa pamoja kwa kuhusianisha na Halmashauri inavyotekeleza majukumu yake.

### 2.1.1 MIPAKA NA JIOGRAFIA

Wilaya ina eneo la kilomita za mraba 2,523. Inapatikana magharibi ya Ziwa Victoria kati ya longitudo $30^0$ 48' na $31^0$ 49' mashariki na latitudo $1.0^0$ 00' na $10^0$ 30' kusini. Kwa upande wa Kaskazini Wilaya ya Missenyi inapakana na Uganda, Ziwa Victoria upande wa mashariki na sehemu ya Halmashuri ya Wilaya Bukoba. Upande wa kusini inapakana na Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba wakati upande wa magharibi inapakana na Halmashauri za Wilaya za Karagwe na Kyerwa.

Kwa ujumla Wilaya inapata mvua za kutosha kwa takribani misimu miwili katika mwaka kati ya Oktoba na Novemba (msimu mfupi) na kati ya Machi na Mei (msimu mrefu). Mvua kwa mwaka zinanyesha kwa wastani wa kati ya milimita 1,400 na 2000; ukanda wa nyanda za juu ni kati ya milimita 1,000 na 1,400; eneo la magharibi ni kati ya milimita 600 na 1,000. Joto la wastani ni $20^0$ C ambapo huongezeka kufikia kati ya nyuzi joto $15^0$C na $28^0$C.

### 2.1.2 UTAWALA

Kiutawala, Wilaya ya Missenyi imegawanyika katika Tarafa mbili na Kata 20 zenye Vijiji 77 na Vitongoji 356 (Jedwali Na.1.2). Kwa upande wa eneo la ardhi, Tarafa ya Missenyi imechukua sehemu kubwa ya ardhi katika Wilaya (71.5%), na Tarafa ya kiziba inabaki na 27.9% ya jumla ya ardhi yote.

**Jedwali Na.1 Maeneo ya Kiutawala katika Wilaya ya Missenyi.**

| Tarafa | Eneo la Ardhi(km$^2$) | Idadi ya Kata | Idadi ya Vijiji | Idadi ya Vitongoji | Asilimia ya eneo la Ardhi |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kiziba** | 774.0 | 10 | 43 | 178 | 27.9 |
| **Missenyi** | 1,749.0 | 10 | 31 | 178 | 71.5 |
| **Jumla** | **2,523** | **20** | **77** | **356** | **100** |

**Chanzo:**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (Idara ya Utawala), Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, 2020

### 2.1.3 IDADI YA WATU

Wilaya ya Missenyi kwa takribani miaka kumi iliyopita kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu. Kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Wilaya ya Missenyi ilikuwa na jumla ya watu 202,632 kati ya hao, wanawake 102,547 (52%) na wanaume 100,085 (48%).

### 2.1.4 HALI YA UCHUMI YA WILAYA

Uchumi wa wananchi wa Missenyi unategemea Zaidi kilimo na ufugaji. Inakadiriwa kuwa Zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wanajishughulisha na kilimo. Shughuli zingine za kiuchumi ni biashara, ufugaji nyuki, mazao ya misitu, uchimbaji madini, uvuvi na shughuli za mikono.

### 2.1.5 KILIMO

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Wilaya ya Missenyi na asilimia kubwa ya wakazi wake wanategemea kilimo kama chanzo kikuu cha kujikimu kimaisha. Kilimo kinafanyika katika kata zote za Wilaya ya Missenyi.Wilaya ya Missenyi ina eneo la ardhi lenye jumla ya hekta 270,875 ambapo eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 105,298.43 (38.9%). Eneo linalotumika kwa kilimo ni Hekta 53,532.1 sawa na asilimia 50.8 ya eneo linalofaa kwa kilimo.

### 2.1.6 MIFUGO

Ufugaji ni shughuli ya pili muhimu ya kiuchumi baada ya kilimo.aina ya mifugo inayofugwa katika Wilaya missenyi na makadirio yake kwa idadi ni ng'ombe (67,820) ,mbuzi (28,200), kondoo (3,839) na nguruwe (7,961). Kuku wa kienyeji (56,800) ni wengi zaidi ya kuku wa nyama na mayai (2,104).

**Jedwali Na.2: Mgawanyo wa Mifugo katika Wilaya ya Missenyi.**

| Ng'ombe | | | Mbuzi | | Kondoo | Kuku | Nguruwe | Sungura |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| kienyeji | Maziwa | Nyama | Kienyeji | Maziwa | | | | |
| 64,890 | 1,202 | 2,607 | 26,609 | 2,170 | 3,839 | 56,800 | 7,961 | 2,791 |

**Chanzo:** Sensa ya mifugo Wilaya ya Missenyi 2019

### 2.1.7 NYUKI

Wilaya ya Missenyi ina mizinga ya asili 1,637. Kata ya Kyaka ina idadi kubwa ya mizinga ya asili 284 wakati Kata za Buyango, Ishozi, Kashenye, Bugorora na Ishunju hazina mizinga ya asili.

### 2.1.8 UVUVI

Shughuli kubwa za uvuvi katika Wilaya ya Missenyi zinafanyika katika Kata ya Kashenye. Wilaya ya Missenyi ina eneo dogo la maji ya Ziwa Victoria lakini bado halijatumika kikamilifu kutokana na kutokuwepo na sehemu za masoko ya samaki na miundombinu mizuri. Wilaya ina wavuvi 173 na mitumbwi 62.

### 2.1.9 UTALII

Wilaya ya Missenyi ni moja ya Wilaya katika Mkoa wa Kagera ambayo imejaliwa kuwa na vivutio vingi vya utalii. Hii ni kutokana na hifadhi za kitaifa ambazo hutoa huduma za utalii wa picha, kutembelea na majini kutumia boti. Wilaya pia ina makabila ya aina mabalimbali yanayochangia na kunufaika na utalii. Mbali na kujaliwa vivutio vingi, Wilaya ya Missenyi kwa kuwepo pembezoni magharibi inatembelewa na watalii wachache ikilinganishwa na Wilaya zingine zilizopo upande wa Kaskazini na Kusini.

### 2.1.10 HUDUMA ZA AFYA

Wilaya ya Missenyi imeendelea kuimarika katika sekta ya afya kwa kujenga sehemu za kutolea huduma za Afya hasa zahanati na vituo vya Afya. Wilaya inavyo vituo vya kutolea huduma za afya zikiwemo Hospitali 2, Vituo vya afya 3 na Zahanati 32. Sekta binafsi pia zina mchango mkubwa katika utoaji wa huduma za afya ambapo kuna vituo 11 (hospitali 2, kituo vya afya 1 na zahanati 6) zinazomilikiwa na sekta binafsi wakati sehemu za huduma 25 (kituo cha afya 1 na zahanati 24) zinamilikiwa na Serikali.

**Jedwali Na.3 sehemu za huduma za Afya zilizopo**

| **Sehemu za kutolea huduma** | **Umiliki** | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Serikali** | **Mashirika ya Dini** | **Shirika la umma** | **Shirika Binafsi** | |
| Hospitali | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 |
| Kituo cha afya | 2 | 1 | 0 | 0 | 3 |
| Zahanati | 26 | 4 | 1 | 1 | 32 |
| **Jumla** | **28** | **6** | **1** | **1** | **37** |

**Chanzo:** Rejista ya Sehemu za kutolea huduma za Afya, 2018

### 2.1.11 SEKTA YA ELIMU

#### 2.1.11.1 ELIMU YA MSINGI

Wilaya ya Missenyi in jumla ya Shule za msingi 107, kati ya hizo 96 zinamilikiwa na Serikali na 11 zinamilikiwa na sekta binafsi. Jumla ya wanafunzi waliopo ni 46,168 kati yao 23,391 wavulana na 22,777 wasichana.

#### 2.1.11.2 ELIMU YA SEKONDARI

Wilaya in shule za Sekondari 27, kati ya hizo 22 zinamilikiwa na Serikali, 5 zinamilikiwa na sekta binafsi. Jumla ya wanafunzi katika shule za Sekondari ni 11,523 ambapo 5,453 ni wanaume na 6,079 wanawake. Wilaya ina taasisi za mafunzo 2 ambazo ni kituo cha uuguzi kinachopatikana Hospitali ya Mughana na taasisi ya mafunzo ya ufundi Gera.

### 2.1.12 MAMLAKA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI

Kama ilivyo kwa Halmashauri zingine Tanzania, Halmashauri ya Wilaya Missenyi inaendeshwa kisheria kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopitishwa na bunge chini ya Sheria ya Serikali za mitaa Na. 8 ya Mwaka 1982. Katika Sheria hii Halmashauri ya Wilaya inawajibu wa majukumu muhimu kama ifuatavyo;

i. Kusimamia na kuwezesha uwepo wa Amani, utaratibu na utawala bora katika eneo la mipaka yake ya kiutawala
ii. Kuendeleza ustawi wa jamii na uchumi bora kwa watu katika eneo la mipaka yake ya kiutawala kulingana na sera za nchi na mipango ya maendeleo ya mijini na vijijini
iii. Kuimarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika eneo lake la kiutawala
iv. Kuchukua hatua madhubuti kulinda na kuendeleza mazingira ili kuchochea maendeleo endelevu
v. Kusimamia ugatuaji wa madaraka katika masuala ya siasa,fedha na uongozi kuhusiana na majukumu,madaraka,uwajibikaji na utoaji huduma katika ngazi zote za Mamlaka za Serikali za mitaa.
vi. Kuendeleza na kuhakikisha demokrasia inakuwepo katika kushiriki na kusimamia utoaji wa maamuzi kwa watu wake.

## 2.2 MAPITIO YA UTEKELEZAJI

| Na. | Lengo mahsusi | Shabaha | Mafanikio |
|---|---|---|---|
| | **1. Elimu Sekondari** | | |
| 1.1 | Huduma zimeimarika na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI yamepungua | Ufahamu kuhusu maambukizi ya virusi vya UKIMWI /UKIMWI uongezeke na kupunguza mila potofu kutoka 2% hadi 1.5% katika Shule za Sekondari 27 ifikapo juni 2023 | Mila potofu kuhusu UKIMWI/Virusi vya UKIMWI zimepungua kufikia 1.5% kupitia semina elekezi za ufahamu kwa wanafunzi na walimu |
| 1.2 | Mkakati juu ya kupambana na rushwa kitaifa | Ufahamu kuhusu kampeni dhini ya mapambano ya rushwa kwa wanafunzi na walimu katika shule za | Klabu hai 27 kwa wanafunzi wa sekondari zimejengewa uwezo juu ya kupambana na rushwa katika jamii |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | umewezeshwa na kuendelezwa | sekondari 27 uongezeke ifikapo juni 2023 | |
| 1.3 | Upatikanaji wa huduma za jamii bora na zenye usawa umeongezeka | Ufaulu kwa mitihani ya Kidato cha pili,nne na sita uongezeke kutoka 76% hadi 96% ifikapo juni,2023 | Ufaulu wa kidato cha pili umeongezeka kutoka 76% - 86%,kidato cha nne kutoka 76% - 78% na kidato cha sita kutoka 99% - 100% |
| | | Ufahamu kwa walimu juu ya kanuni na majukumu yao uongezeke kutoka 78% - 96% kwa walimu wa sekondari 395 ifikapo juni,2023 | Uwajibikaji kwa walimu umeongezeka |
| | | Ujuzi katika uongozi na menejimenti kwa shule za sekondari uhimarishwe kutoka 82% - 93% ifikapo juni 2023 | Ujuzi juu ya menejimenti na uongozi umetolewa kwa walimu Wakuu 27 |
| | | Kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za ufundishaji na kujifunza kutoka 76% - 98% ifikapo juni 2023 | Kiwango cha kitaaluma kimeboreshwa |
| | | Satahiki za Walimu wa Sekondari zimewezeshwa kutoka 70% - 91% ifikapo juni 2023 | Walimu wa Sekondari 142 wamelipwa posho za likizo |
| | Ubora na idadi ya miundombinu na huduma za kiuchumi umeongezeka | Miundombinu ya shule iongezeke kutoka 58% - 78% kwa shule za sekondari 27 ifikapo juni 2023 | Idadi ya Madarasa imeongezeka kutoka 215 hadi 247, maabara kutoka 7 hadi 49 na matundu ya vyoo kutoka 311hadi 335. |
| | **2. Elimu Msingi** | | |
| 2.1 | Upatikanaji wa huduma za jamii bora na zenye usawa umeongezeka | Kiwango cha uandikishaji wanafunzi shule za awali na msingi kiongezeke kutoka 98% hadi 99% ifikapo juni 2023. | • Mwaka 2018 wanafunzi walioandikishwa shule za awali ni 5,692 (wav.3,193,na was.2,499)<br>• Mwaka 2020 wanafunzi walioandikishwa shule za awali ni 6,403( wav.3,119 na was.3,284) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | • Mwaka 2020 Wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza 5,841(wav.2,861 na was.2,980)sawa na 97.67%. |
| | | Kiwango cha ufaulu kwa darasa la nne kiongezeke kutoka 97% - 99% na darasa la saba kutoka 84% - 95% ifikapo juni,2023 | Kiwango cha ufaulu kimeongezeka kutoka mwaka 2018 ambapo darasa la saba wanafunzi waliosajiliwa ni 4,042(Wav. 1,968 na Was.2,074) , waliofanya mitihani ni 4,028(Wav. 1,962 na Was.2,066), waliofaulu mitihani ni 3,417(Wav. 1,619 na Was.1,798) sawa na 84.41% ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo wanafunzi waliosajiliwa darasa la saba ni 4,545(Wav. 2,288 na Was.2,257) walifanya mitihani ni 4,500(Wav.2,270 na Was. 2,230). Waliofaulu mithiani ni 4,055(Wav.2,018,Was.2,037) sawa na 90.11% na wote walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza |
| | | Ushiriki wa michezo kati ya wanafunzi na vijana katika Wilaya ya Missenyi uongezeke kutoka 56% hadi 78% ifikapo juni 2023 | Tumeratibu na kuwezesha uanzishaji na kusajili klabu 3 za wanaume za mpira wa miguu na klabu 1 ya wanawake ya mpira wa miguu katika Wilaya. |
| | | Shughuli za kitamaduni katika Wilaya ya Missenyi zihimarishwe kutoka 65% hadi 85% ifikapo juni 2023 | Maeneo 7 ya utalii yametambuliwa na wanajamii wamehamasishwa kulinda maliasili(Kanyigo,Bwanjai,Bugandika ,Buyango na Bunazi) |
| | | Kupunguza kutojua kusoma na kuandika kwa watu wazima kutoka 38% hadi 17% ifikapo juni 2023 | Vituo 10 vya kujifunzia watu wazima(COBET) vimeanzishwa ambapo wanafundishwa na kujifunza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | masuala mbalimbali ya kielimu ikiwemo 3R |
| | Huduma zimeimarika na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI yamepungua | Ufahamu kuhusu maambukizi ya virusi vya UKIMWI /UKIMWI uongezeke kutoka 96% hadi 98% kwa walimu 746 katika Shule za Msingi 96 ifikapo juni 2023 | Walimu 2 kutoka kila shule wamehudhuria semina kama wawakilishi katika shule walizotoka na kwenda kuwajengea uwezo walimu wote katika shule zao |
| | Mkakati juu ya kupambana na rushwa kitaifa umewezeshwa na kuendelezwa | Ufahamu kuhusu kampeni dhini ya mapambano ya rushwa kwa walimu 746 katika shule za Msingi 96 uongezeke ifikapo juni 2023 | Walimu 2 kutoka kila shule wamehudhuria semina kama wawakilishi katika shule walizotoka na kwenda kuwajengea uwezo walimu wote katika shule zao |
| | Ubora na idadi ya miundombinu na huduma za kiuchumi imeongezeka | Miundombinu ya shule 96 za msingi iongezeka kutoka 79% hadi 85% ifikapo juni 2023 | Miundombinu imeongezeka ambapo;<br>• Madarasa yameongezeka kutoka 657(2015) hadi 764(2020)<br>• Madawati yameongezeka kutoka 14,022(2015) hadi 19,111(2020)<br>• Matundu ya vyoo yameongezeka kutoka 1,026(2015) hadi 1,296(2020)<br>• Zimejengwa Nyumba za walimu 199 katika Wilaya. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Huduma za uongozi na Utawala bora zimehimarishwa | Mazingira ya kazi kwa walimu yahimarishwe kutoka 98% hadi 99% ifikapo juni 2023 | • Ulipaji wa stahiki za walimu kama vile likizo, uhamisho, kuwezeshwa kuhudhuria semina za kitaaluma.Mfano posho za likizo;<br>• Mwaka 2018 walimu 189 walilipwa kiasi cha Tsh.37,957,000<br>• Mwaka 2019 walimu 137 walilipwa Tsh.27,895,000<br>• Mwaka 2020,walimu 105 walilipwa kiasi cha Tsh.23,803,00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **3. Mifugo na Uvuvi** | | |
| **3.1** | Upatikanaji wa huduma za jamii bora na zenye usawa umeongezeka | Shughuli za ufugaji zihimarishwe kutoka 65% hadi 85% katika kata 20 ifikapo 2023 | Ng'ombe 82,335 wamesajiliwa na kutambuliwa kwa kupigwa chapa sawa na 70%, makundi ya wafugaji 4 yamepewa mafunzo ya uongozi na kuunda ushirika na huduma za ugani. Mafunzo yametolewa kwa wafugaji 183 kuhusu malisho bora pamoja na kupatiwa vifaa 5,500 vya kukatia majani ya malisho na miti ya lishe 5000. Aidha, mashine 2 za mbegu za malisho zimenunuliwa. |
| | | Shughuli za uvuvi katika Kata 20 ziwezeshwe kutoka 60% hadi 80% ifikapo juni,2023 | Wavuvi 370 wamepatiwa mafunzo juu ya ujenzi wa mabwawa, doria 18 zimefanyika ziwa Victoria ili kudhibiti uvuvi haramu pamoja na kutoa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | mafunzo ya njia bora za uvuvi. Mafanikio ni asilimia 65 |
| **3.2** | Ubora na idadi ya miundombinu na huduma za kiuchumi imeongezeka | Huduma za afya ya mifugo zihimarishwe kutoka 60% - 80% katika Kata 20 ifikapo juni,2023 | Huduma za afya ya mifugo zimehimarishwa kwa 65% kupitia chanjo kwa ng'ombe 42,031(CBPP,Branthrax,FMD,Rabies na lamp skin), uhamilishaji wa ng'ombe 1,283 na mafunzo ya para – vet kwa wafugaji wadogo 4 yamefanyika katika kituo cha wakala wa mafunzo ya mifugo Kikulula |
| | | Miundombinu ya ufugaji katika Kata 20 ihimarishwe kutoka 65% hadi 80% ifikapo juni,2023 | Ofisi moja imejengwa katika soko la mifugo la Mutukula,matundu 2 ya vyoo yamejengwa katika soko la mifugo Bubale, ukarabati wa majosho 3(kihororo,Omukato na Kamashasha).mafanikio ni asilimia 70 |
| | | Miundombinu ya uvuvi katika Kata ya Kashenye ihimarishwe kutoka 60% hadi 90% ifikapo juni,2023 | Bwawa 1 la samaki limejengwa kijiji cha Kikono,matundu 4 ya vyoo yamejengwa katika mwalo wa Kabindi |
| **3.3** | Huduma mtambuka za lishe zime himarishwa | Kuongeza idadi ya kaya zilizohamasishwa juu ya umuhimu wa kula vyakula vyenye lishe kutoka 45% hadi 80% ifikapo juni,2023 | Limetekelezwa kwa asilimia 60. Mafunzo yamefanyika katika Kata ya Kiziba kwa watu 533 juu ya ufugaji wa samaki na kuku na watu 230 wamepatiwa mafunzo juu ya ufugaji wa mbuzi na ng'ombe wa maziwa.yote hayo yamehamasisha ulaji wa mayai, samaki na unywaji maziwa.waishio na virusi vya UKIMWI 68 kata ya Kiziba wamewezeshwa mbuzi wa maziwa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **4. Ardhi na Maliasili** | | |
| **4.1** | Usimamizi wa maliasili na mazingira umewezeshwa | Ujuzi wa kiufundi katika usimamizi na matumizi ya wanyamapori kwa vijiji 52 uhimarishwe ifikapo juni,2023 | • Mafunzo juu ya mgogoro kati ya binadamu na Wanyamapori yamefanyika kwa Kata 2 ili kusaidia kuimarisha ushirikiano kati ya binadamu na wanyamapori vijiji vya Kakindo na Minziro.<br>• Doria 22 zimefanyika kudhibiti wanyama Wakali katika kata 9 za Kyaka,Kassambya,Minziro,Bugandika,Nsunga,Bubale,Kashenye,Bugorora na Buyango. |
| | | Usimamizi na matumizi ya rasilimali za misitu katika vijiji 52 uhimarishwe ifikapo juni 2023 | • Jumla ya miti 1,500,000 imepandwa katika Kata za Bugorora, Kassambya, Kashenye, Kanyigo, Nsunga, Kitobo, Bugandika, Gera na Bwanjai.<br>• Vitalu 8 vya miche vimeanzishwa katika vijiji vya Kabwoba,Byamutemba,Bunazi,Kyaka na Bugorora |
| **4.2** | Ubora na idadi ya miundombinu na huduma za kiuchumi imeongezeka | Makazi bora (yaliyopangwa) katika maeneo ya Kyaka – Bunazi na Mutukula yaendelezwe ifikapo juni 2023 | Jumla ya michoro 5 ya mipango miji imepitishwa kwa ajili ya utekelezaji maeneo ya Kyaka – Bunazi(4) na Mutukula(1) |
| | | Viwanja 2500 viwe vimehakikiwa,kupimwa na kuwekewa mipaka ifikapo juni,2023 | • Jumla ya viwanja 1013 vimehakikiwa, kupimwa na kuwekewa mipaka katika maeneo ya Kyaka – bunazi na Mutukula. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Hati miliki za mashamba na viwanja ziwe zimeandaliwa na kusajiliwa ifikapo juni,2023 | • Hati miliki 250 zimesajiliwa<br>• Hati miliki za wateja 211 zimesajiliwa |
| | **5. Sheria** | | |
| **5.1** | Huduma za uongozi na Utawala bora zimehimarishwa | Haki za kisheria za Halmashauri katika Kata 20 zinatekelezwa kutoka 70% hadi 95% kufikia juni 2023 | Imefikiwa kwa asilimia 80 kwa kufanyika yafuatayo;<br>• Kupeleka mahakamani na kushinda kesi 16 za Halmashauri.<br>• Kurekebisha Sheria ndogo 7 za makusanyo ya Halmashauri ili kuendana na mahitaji ya sasa.<br>• Mahakama za Kata 20 zimeanzishwa,kusimamiwa na kuwezeshwa kwa kupatiwa miongozo ya kisheria ya kufanyia kazi<br>• Mikataba 145 ya Halmashauri na Vijiji imehakikiwa kabla ya utekelezaji<br>• Watu 71 wamepatiwa msaada wa kisheria bure |
| | | Mazingira ya kazi yawezeshwe kutoka 50% hadi 80% ifikapo juni,2023 | Imefanikiwa kwa asilimia 80 kwa kufanyika yafuatayo;<br>• Mtumishi 1 amewezeshwa kwenda mafunzo ya muda mrefu<br>• Stahiki za kisheria zimelipwa kwa watumishi |
| | **6. Fedha na Biashara** | | |
| **6.1** | Upatikanaji wa huduma za jamii bora na zenye | Kanuni na miongozo ya kifedha katika Halmashauri isimamiwe kikamilifu ifikapo juni,2023 | Idadi ya hoja za ukaguzi imepungua kutoka 15% (2019/2020) ikilinganishwa na 2018/2019 ambapo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | usawa umeongezeka | | ilikuwa 11% na muhimu zaidi miongozo ya fedha inapatikana ya kutosha katika idara.Aidha, kiwango cha faini na adhabu kwa makosa yanayofanywa na wafanyabishara binafsi kimepungua. |
| | | Uelewa wa sheria na kanuni kwa wafanyabiashara wote uwe umeongezeka kutoka 80% hadi 90% kufikia juni,2023 | Uelewa wa sheria na kanuni za biashara umeongezeka kwa 84% (2019/2020) kutoka 80% (2018/2019) kutokana na elimu ya mara kwa mara inayotolewa kwa wafanyabiashara wanapokuja kuhudumiwa na kupitia vikao pekee vya kibiashara vinavyofanyika mara 2 kwa mwaka. |
| | | Makusanyo ya mapato ya Halmashauri yaongezeke kwa 16% ifikapo juni,2023 | Mapato ya vyanzo vya ndani yameongezeka kwa 13% sawa na Tsh 327,613,695 ya ongezeko (ambapo kiasi cha mapato halisi yaliyokusanywa mwaka 2019/2020 ni Tshs 2,795,226,695) ikilinganishwa na mwaka 2018/19 Tshs.1,891,744,687 ya mapato ilikusanywa chini ya makisio ya bajeti. |
| | **7. Ukaguzi wa ndani** | | |
| **7.1** | Huduma za uongozi na Utawala bora zimehimarishwa | Mifumo ya fedha,taarifa na ukaguzi ya halmashauri iboreshwe kutoka 85% hadi 90% kufikia juni,2023 | Mifumo ya uhasibu na ukaguzi imeboreshwa kutoka 85% hadi 88% na umeweza kufanya yafuatayo;<br>• Ukaguzi wa mapato na matumizi kwa idara 10 na vitengo 5<br>• Ukaguzi wa Miradi ya maendeleo; SWASH,EP4R,SEDIP II,UNDP |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Mazingira ya kazi yawezeshwe kutoka 50% hadi 80% ifikapo juni,2023 | Shabaha imefikiwa kwa asilimia 75. Yafuatayo yamefanyika;<br>• Watumishi wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu<br>• Vifaa na matumizi ya ofisi vimelipwa. |
| | **8. Teknolojia na habari** | | |
| **8.1** | Upatikanaji wa huduma za jamii bora na zenye usawa umeongezeka | Usimamizi wa mifumo ya teknolojia na habari uhimarishwe ifikapo juni 2023 | Usimamizi wa mifumo ya teknolojia na habari umehimarika kwa asilimia 85 |
| | | Utoaji wa taarifa kupitia tovuti uhimarishwe kutoka 50% hadi 90% ifikapo juni 2023 | Kwa wastani 65% ya taarifa za kijamii zinapatikana katika tovuti ya Halmashauri |
| **8.2** | Ubora na idadi ya miundombinu na huduma za kiuchumi imeongezeka | Miundombinu ya mtandao wa ndani wa Halmashauri iboreshwe ifikapo juni,2023 | Imetekelezwa kwa asilimia 70 ambapo ofisi za halmashauri karibu zote zinatumia mfumo wa LAN |
| | | Mazingira ya kazi kwa watumishi 2 yawezeshwe ifikapo juni,2023 | Watumishi 2 wamehudhuria mafunzo kuhusiana na ICT |
| | | Upatikanaji wa vifaa vya teknolojia uboreshwe kutoka 50% hadi 80% | Vifaa vimenunliwa na vipo kwa uhakika wa 100% |
| | **9. Maendeleo ya Jamii** | | |
| **9.1** | Maendeleo ya jamii,jinsia na uwezeshaji jamii umehimarishwa | Uhamasishaji katika kata 20 kwa kutatua changamoto na kuweka mikakati ya utatuzi wa changamoto zijazo kwa kutumia rasilimali zilizopo ufanyike ifikapo juni 2023 | Miradi inayoibuliwa na jamii imewezeshwa katika kata 7. Miradi hiyo ni; ujenzi wa bwalo sekondari ya Bwabuki,miradi ya maji(vijiji vya Igurugati,Kashaba,Bulembo,Kenyan a,Nyankere) , madarasa Bunazi sekondari,Bunazi Shule ya Msingi( |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Bunazi A na B – Kabwera) na Kabakesa. |
| | | Uelewa wa jamii kuhusu mila potofu,mazoea na Imani za kishirikina ambazo zinazuia maendeleo upatiwe ufumbuzi ifikapo juni 2023 | Vipindi 6 vyaRadio kuhusu elimu ya jamii (radio Karagwe FM,Radio FADECO na Quizera FM),kampeni 1 dhidi ya mimba na UKIMWI vimefanyike katika Kata 20 |
| | | Uhamasishaji wa jamii katika kuanzisha na kuendeleza vikundi vya kijamii vya wanawake na watoto viwezeshwe ifikapo juni,2023 | Vikundi vya kijamii 262(wanawake vikundi 158, vijana vikundi 91 na wenye ulemavu vikundi 13) vimeanzishwa na kuendelezwa |
| | | Elimu katika jamii kuhusu sera ya watoto,jinsia na maendeleo ya jamii iwezeshwe katika Kata 20 ifikapo juni,2023 | Wastani wa watu 202,632 wamefikiwa na kuhamasishwa kupitia mikutano ya hadhara katika kata 20 |
| | | Kaya maskini 6,292 kutoka vijiji 50 zipatiwe msaada wa TASAF ifikapo juni 2023 | • Kaya maskini 6,292 zimenufaika na msaada wa TASAF ambapo kiasi cha Tshs. 5,141,704,500 zimetolewa kupitia program hiyo.<br>• Kaya maskini 3,267 zinatekeleza miradi ya kujiingizia kipato |
| | | Shughuli za mashirika binafsi zinazotekelezwa katika Wilaya ziratibiwe na kusimamiwa ifikapo juni 2023 | Mashirika binafsi 18 yanayofanya kazi katika Wilaya katika sekta za Afya,kilimo,Elimu,uwezeshaji uchumi) yanaratibiwa na kusimamiwa |
| | **10. Afya** | | |
| **10.1** | Huduma zimeimarika na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI yamepungua | Asilimia ya huduma inayotolewa majumbani kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI iongezeke kutoka 72% hadi 90% ifikapo juni 2023 | Asilimia ya huduma inayotolewa majumbani kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI imeongezeka kutoka 85% hadi 90% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kiwango cha Maambukizi ya UKIMWI kipungue kutoka 6.4% hadi 1% ifikapo juni 2023 | Kiwango cha Maambukizi ya UKIMWI kimepungua kutoka 6.0% hadi 1% |
| **10.2** | Upatikanaji wa huduma za jamii bora na zenye usawa umeongezeka | Uhaba wa madawa,vifaa tiba na vifaa vya uchunguzi upungue kutoka 20% hadi 10% ifikapo juni 2023 | Uhaba wa madawa,vifaa tiba na vifaa vya uchunguzi umepungua kutoka 19% hadi 10% |
| | | Mapambano dhidi ya Kiwango cha Maambukizi ya kifua kikuu yaongezeke kutoka 22% hadi 60% kufikia juni,2023 | Mapambano dhidi ya Kiwango cha Maambukizi ya kifua kikuu yameongezeke kutoka 33% hadi 60% |
| | | Kiwango cha maambukizi ya malaria kipungue kutoka 35% hadi 20% ifikapo juni,2023 | Kiwango cha maambukizi ya malaria kimepungua kutoka 33% hadi 20% |
| | | Upungufu wa wataalamu katika idara ya afya upungue kutoka 58%hadi 40% ifikapo juni 2023 | Upungufu wa wataalamu katika idara ya afya umepungua kutoka 54% hadi 40% |
| | **11. Kilimo umwagiliaji na ushirika** | | |
| **11.1** | Ubora na idadi ya miundombinu na huduma za kiuchumi na kijamii vimeongezeka | Uzalishaji wa mazao ya chakula kuongezeka kwa wastani wa asilimia 50% ifikapo June 2023 | • Matumizi ya mbolea za viwandani yameongezeka kutoka Tani 91.2 mwaka 2015/16 hadi kufikia Tani 114 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 25<br>• Kiwango cha uzalishaji wa mazao ya chakula kimeongezeka kutoka Tani 152,886 mwaka 2015/16 hadi Tani 202,544.3 mwaka 2019/20<br>• Uzalishaji wa vanilla umeongezeka kutoka Tani 40,401 (mwaka 2015) mpaka 101,111 (2020) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | • Zao la mpunga limeongezeka kutoka Hekta 12 (2015) hadi Hekta 39.4 (2020)<br>• Uzalishaji wa zao la alizeti umeongezeka kutoka Hekta 12 mwaka 2015 hadi Hekta 31 |
| | | Uzalishaji wa mazao ya biashara/kimkakati kuongezeka kwa wastani wa asilimia 50% ifikapo June 2023 | • Uzalishaji wa zao la miwa umeongezeka kutoka Tani 70,028.5 mwaka 2015/16 hadi kufikia Tani 80,000 mwaka 2019/2020<br>• Uzalishaji wa zao la kahawa umeongezeka kutoka Tani 428.9 kwa mwaka 2015/2016 mpaka kufikia tani 910.8 kwa mwaka 2019/20<br>• Idadi ya wakulima wa miwa wa wanje (Outgrowers) imeongezeka kutoka 362 (2015/16) mpaka 525 (2019/20)<br>• Uzalishaji wa miwa umeongezeka kutoka tani 70,028 (2015/16) mpaka kufikia Tani 80,000 (2019/2020) |
| | | Idadi ya miundo mbinu ya kuhifadhi mazao kuongezeka kutoka maghala 3 mpaka 5 ifikapo Juni 2023 | • Maghala 2 ya Mushasha na Kilimilile yenye uwezo wa kuhifadhi Tani 40 za nafaka yamekarabatiwa na ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 20 za nafaka limejengwa katika kata ya Kassambya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Utoaji wa huduma bora za ugani umeongezeka kutoka vijiji 40 mpaka 60 ifikapo Juni 2023 | • Idadi ya maafisa ugani imeongezeka kutoka 25 mwaka 2015/16 hadi 30 mwaka 2019/20<br>• Wakulima wamewezeshwa kushiriki maonesho ya nanenane kimkoa na kikanda na Halmashauri imeweza kushinda miaka 4 mfururizo. |
| | -do- | Mapato ya halmashauri kutokana ushuru wa mazao yameongezeka kwa asilimia 20% ifikapo Juni 2023 | • Wakulima wa miwa wa nje wameweza kulipa ushuru (crop cess) kutoka TZS 32,703,328.18 (2015/16) mpaka 144,000,000 (2019/20) |
| | -do- | Uzalishaji wa mazao ya mbogamboga umeboreshwa katika kata zote 20 ifikapo Juni, 2023 | • Kilimo cha mbogamboga kimeboreshwa kupitia ujenzi wa kitalu nyumba "Greehouse" chenye thamani ya TZS 26,000,000 |
| **11.2** | Huduma mtambuka za lishe zime himarishwa | Upatikanaji na ulaji wa vyakula vyenye viini lishe vingi umeongezeka kutoka 10% mpaka 30% ifikapo Juni 2023. | • Wakulima 120 wamewezeshwa kupata malando bora ya viazi lishe 51,560<br>• Shule 5 za msingi za Mabale, Kenyana, Mabuye, Buchurago & Ruhija zimewezeshwa kupata mbegu bora za maharage lishe. |
| | -do- | | • Hatua ya kuendeleza mnyororo wa thamani wa mazao imeboreka kupitia upatikanaji wa mashine 4 za kupura na kuoboa, mashine 2 za kuchakata, mashine moja ya kukamua mafuta ya alizeti, mashine 1 ya kusaga na kukoboa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | na mashine 4 za kukausha kwa kutumia Jua |
| | -do- | Idadi ya vyama vya ushirika vinavyo fanya kazi kwa ufanisi kuongezeka kutoka 74 mpaka 81 ifikapo Juni, 2023 | • Idadi ya vyama vya ushirika imeongezeka kutoka vyama 73 mwaka 2015/2016 mpaka vyama 78 mwaka 2019/20<br>• Vikundi 9 vya kuweka na kukopa vimewezeshwa kupata mafunzo na vifaa vya kutendea kazi (VSLA kits). Wastani wa mitaji ya vikundi hivi umefikia TZS 4,000,000. Vikundi vimekuwa na uwezo wa kuwekeza kwenye kilimo na biashara |
| | | | |

### 2.3 changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango Mkakati uliopita

**a)** Uswagaji holela wa mifugo katika maeneo ya mipakani
**b)** Uhaba wa fedha za ufuatiliaji na tathmini
**c)** Uhaba wa vitendea kazi vya ofisi na shajala
**d)** Mabadiliko ya sera yanayoathiri vyanzo vya mapato ya Halmashauri
**e)** Mvua za muda mrefu zinazonyesha
**f)** Wanafunzi kuacha shule; uhaba wa walimu. Aidha, uhaba wa miundombinu ya shule ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi waliosajiliwa katika shule husika
**g)** Uchangiaji mdogo wa jamii katika ujenzi wa miundombinu ya shule
**h)** Ulipaji hafifu wa mikopo kwa wanufaika
**i)** Kukosa uwazi katika uwajibikaji kwa baadhi ya wadau

### 2.4 Utatuzi wa changamoto

a) Kampeni za mara kwa mara na kidhibiti uswagaji holela wa mifugo
b) Kuwafundisha wafugaji kupanda nyasi katika mashamba yao
c) Kuwatambua na kwasajili wafugaji na mifugo

d) Kuajiri walimu wa kutosha kukamilisha majukumu yao; kuwahamasisha jamii na wadau kuchangia ujenzi wa miundombinu;kuhakikisha shule zina miundombinu ya kutosha kulingana na idadi ya wanafunzi waliosajiliwa
e) Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara, kutoa notisi kabla kuchukua hatua za kisheria; kuchukua sheria

**2.5 Uchambuzi wa mazingira**

Uchambuzi huu wa mazingira umezingatia mapendekezo na mapitio ya makundi na taasisi tofauti ambazo kuwepo kwao kunaweza kuathiri maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya Missenyi Uchambuzi huu umewezesha Halmashauri kutambua wadau wake na mahitaji yao. Pia uchambuzi umewezesha kupatikana kwa mambo ya msingi ambayo yanaeleza vizuri uwezo, mapungufu, fursa na changamoto kwenye utekelezaji wa shughuli za maendeleo za Halmashauri ya Wilaya Missenyi.

**2.5.1 Uchambuzi na uainishaji wa wadau wa maendeleo**

Utambuzi wa wadau wa Maendeleo katika halmashauri ya wilaya Missenyi ni muhimu ili kutambua michango yao kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Lengo la utambuzi huu ni kutambua majukumu na matarajio yao. Matarajio ya wadau ni kupata ushirikiano mzuri na sekta ya umma. Uchambuzi wa wadau ulifanyika ili kubaini malengo muhimu ya kushughulikia katika kutatua changamoto na vikwazo vya maendeleo na kuainisha vipaumbele, viwezeshi pamoja na fursa zilizopo za maendeleo

**Jedwali la Wadau wa maendeleo na uwezo, udhaifu, fursa na vitisho linapatikana katika Document kubwa**

**2.6 Mambo muhimu ya kuzingatia/ maeneo muhimu ya matokeo**

Halmashauri ya Wilaya Missenyi ilibaini mambo na maeneo muhimu ya kuzingatia ili kuweza kufikia kiwango tarajiwa cha ukuaji wa uchumi;

**i.** Ushirikishwaji wa jamii katika kufanya maamuzi ya maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.
**ii.** Uzingatiaji wa masuala ya usawa kijinsia

iii. Uwajibikaji, uwazi na uadilifu kwenye usimamizi wa masuala ya umma

iv. Elimu kwa jamii kuhusu fursa zilizopo Wilayani ili waweze kuboresha mazao ya kilimo na mifugo

v. Uwepo wa Amani na Usalama Wilayani

vi. Mapambano dhidi ya ongezeko la maambukizi ya HIV/AIDS na kutoa misaada kwa watoto walio kwenye mazingira magumu

vii. Ushiriki wa wadau kikamilifu kwenye uibuaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya usimamizi wa mazingira

## SURA YA TATU

### 3.0. UTANGULIZI

Sura ya tatu ya mpango inaweka bayana malengo na madhumuni yanayokusudiwa kutekelezwa na H/Missenyi ikiwa ni pamoja na viashiria vitakavyo tumiwa katika kufuatilia na kupima kiwango cha utekelezaji wa malengo hayo.

H/Missenyi ni serikali ya mtaa na hivyo ni chombo cha kutekeleza sera mbalimbali za kisekta katika ngazi za chini za vitogoji, vijiji na kata na huduma zake zinalenga na kugusa wanajamii walio wengi.

Hivyo H/Missenyi kupitia mpango mkakati huu inakusudua kutoa huduma kwa jamii kwa kufuata na kuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya uendeshaji wa serikali za mitaa na vivyo hivyo kuendeleza utekelezaji wa sera kuu za kitaifa na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mpango mkakati huu unatengenezwa na vipengere muhimu (core features) ambavyo vinaweka bayana namna ambavyo mpango utachangia katika kuiwezesha Halmashauri kutekeleza malengo ya maendeleo ya kitaifa  na utaboresha uwezo wa Halmashauri kutoa huduma bora kwa jamii.

Lengo la kutekeleza mpango mkakati ni kuboresha utendaji wa halmashauri katika utoaji wa huduma kwa jamii kwa viwango vinavyoridhisha na hatimaye Halmashauri kuweza kutimiza majukumu yake kama serikali ya mtaa.

Mpango mkakati pia utakuza uwezo wa Halmashuri kutekeleza na kuzingatia mifumo ya kiutawala na kisera (governance and policy framework) katika utoaji wa huduma kwa; serikali na wadau wengine kuwa na wajibu wa kuongeza kiwango cha uwekezaji na uchangiaji wa pesa (funding) kwenye maendeleo ya Halmashauri, kuweka msisitizo kwenye shughuli na miradi yenye gharama ndogo/nafuu (low cost interventions) lakini yenye matokeo makubwa kwenye maendeleo ya Halmashauri (High value for money),

utakuza na kuimarisha mtandao wa mahusiano na serikali za mitaa (strong collaborative networks with LGAs) na Asasi za kiraia (civil societies organizations).

Vipengele vilivyopo katika sura hii pia vinaweka bayana namna ambavyo Halmashauri itawajibika kuteleza mpango mkakati na itazingatia na kuchangia katika kutekeleza program na malengo ya kitaifa.

### 3.1 Dira ya Halmashauri

Dira ya Halmashauri ya wilaya ya Missenyi ni kauli yenye mapana inayoweka bayana sura ya namna ambavyo halmashauri inataka au ingependa kuwa kwa siku za baadaye na inatoa taswira ya malengo ambayo halmashauri inalenga kuyatimiza

Dira ya Halmashauri ya wilaya ya Missenyi inasema kuwa: "Halmashauri ya wilaya ya Missenyi inalenga katika kuboresha na kukuza viwango vya kijamii na kiuchumi vya jamii/watu wake.

Dira hii inatengenezwa na kuongozwa na mihimili mikuu ya maadili (core values) ya uongozi bora (good leadership), ushiriki wa jamii (community participation), usawa (equity), uwazi (transparency), huduma bora (quality service), (kuzingatia mahitaji na vipaumbele vya jamii (responsiveness), maemdeleo endelevu (sustainable development) na uwajibikaji na uondoaji wa kero za jamii (simplicity and accountability).

### 3.2 Dhima

Dhima ya Halmashuri inaweka bayana kwa nini Halmashauri ya wilaya ya Missenyi ipo na nini inacho kifanya/kutekeleza. Inaelezea shughuli kuu ya Halmashauri (core business) na inatoa taswira ya mwelekeo wa kazi na majukumu yake (direction scope of its work).

Dhima ya Halmashauri ya wilaya ya Missenyi inasema kuwa; "Halmashauri ya wilaya ya Missenyi inakusudia kuboresha kiwango cha maisha ya kijamii na kiuchumi cha watu wake/jamii kwa kutumia rasilimali za ndani na nje na kwa kuzingatia misingi ya demokrasia, ushirikishwaji wa jamii na utawala bora katika kuondoa umaskini.

### 3.3 Maadili ya msingi (Core Value)

Maadili ya msingi yanaweka bayana namna ambavyo Halmashauri inakusudia kufanya kazi. Ni miongozo inayotoa sura ya utoaji/ufanyaji wa maamuzi ya siku hadi siku (day to day decisions) wa Halmashauri, tabia na mienendo (attitude and conduct) itakayo tumiwa na kuzingatiwa na Halmashuri ikiwa ni pamoja na mikakati yake na sera zake.

Ili Halmashuri iweze kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii inahitaji kuzingatia na kufuata maadili ya msingi.

Halmashuri itatoa huduma kwa jamii kwa kuzingatia maadili ya msingi yafuatayo

a. Usawa (Equity)
b. Huduma yenye ufanisi/ubora na yenye kuleta matokeo tarajiwa (Efficiency and Effectiveness)

c. Kufanya kazi kwa mashirikiano/timu (Teamwork)
d. Uwajibikaji (Accountability and Responsibility)
e. Uaminifu na weledi katika utoaji wa huduma (Integrity)
f. Huduma bora kwa wateja (Customer care)
g. Uwazi (Transparency)
h. Kuheshimu na kuzingatia utawala wa sheria (Respect rule of law)
i. Kuheshimu na kuzingatia jinsia (Gender)

Mpango mkakati wa Halmashauri ya Missenyi unalenga kujenga mazingira ambayo yataziwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika kupanga na kutekeleza shughuli ambazo zinatarajiwa kukuza na kuboresha viwango vya maisha kama vile vya utosherezi/usalama wa chakula, upatikanaji wa maji safi na salama, upatikanaji wa huduma bora za elimu na afya, miundo bora ya mawasiliano, mazingira bora, uwepo wa demokrasia, haki za jamii na usawa wa kijinsia.

Mpango mkakati umetengenezwa kwa namna ambayo utawezesha jamii za Halmashauri ya Missenyi kutekeleza na kufikia maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

### 3.4 Malengo

Mpango mkakati huu unayo malengo makuu 9 yanayo shabihiana na kusaidiana.

#### 3.4.1 Lengo A: Huduma kuboreshwa na kupungua kwa maambukizi ya VVU

**Viashiria vya ufanisi:**

a) Utambuzi na usajiri wa Maambukizi mapya ya VVU na magonjwa mengine sugu (chronic diseases).
b) Uwepo wa watumishi wa Halmashauri na wanajamii wanaoishi na VVU na magonjwa mengine sugu walio wezeshwa/saidiwa na kupewa huduma na Halmashauri
c) Kukua kwa kiwango cha jamii kusaidia na kuwezesha watu wanao ishi na VVU na magonjwa sugu (chronic diseases infections)
d) Uwepo wa matukio na mafanikio yanayo husiana na VVU yaliyo tolewa taarifa (reported) na kuwekwa katika kumbukumbu (documented).

**Dhanio/wazo la msingi (Basic Assumptions):**

- ❖ Utashi na utayari wa jamii kubadili tabia na mtindo wa maisha.
- ❖ Mabadiliko ya tabia miongoni mwa watu wanaoishi na VVU na wenye VVU kukubalika na kusaidiwa na jamii na kutokuwepo kwa unyanyapaa.
- ❖ Serikalini na Wadau wengine kuendelea kuwezesha na kusaidia na kutoa vipaumbele katika shughuli na progamu za VVU/UKIMWI.

#### 3.4.2 Lengo B: Mpango wa taifa wa kupambana na rushwa kutekelezwa na kuwa endelevu

**Viashiria vya ufanisi**

- ❖ Kampeni za vita dhidi ya rushwa zilizo tekelezwa, kutolewa taarifa na kuwekwa katika kumbukumbu.
- ❖ Taarifa za matukio ya rushwa zilizo andaliwa kwa mwaka.

**Dhanio/wazo la msingi:**

- ❖ Utashi na utayari wa mabadiliko ya kitabia kwa Jamii na watumishi wa Halmashauri.
- ❖ Hakutakuwa na mabadiliko hasi ya mifumo ya kiutawala (governing framework) na mabadiliko ya sera za kitaifa (national policies) yatakayo athiri haki za wananchi za kijamii na kiuchumi (social and economic rights).
- ❖ Serikalini na Wadau wengine kuendelea kuwezesha na kusaidia na kutoa vipaumbele katika kupambana na rushwa na kuendeleza uwajibikaji, uwazi na weledi.

**lengo C:** Usawa katika upatikanaji wa huduma bora za kijamii

**Viashiria vya ufanisi**

- ❖ Vijiji na kata kupewa vitendea kazi na rasilimali muhimu/hitajika
- ❖ Uwepo wa ofisi za uratibu za vijiji na kata zenye rasilimali na vitendea kazi tosherezi.
- ❖ Uwepo wa sheria ndogo, sera za ndani (internal polices) na taratibu za kiuongozi (administrative procedures) zilizo fanyiwa maboresho.
- ❖ Uwepo wa uwazi wa mfumo wa upandishaji vyeo (All outstanding promotion rewards cleared).
- ❖ Bajeti kupewa fedha (budget financing) kwa 100% .
- ❖ Mtiririko wa kazi (Workflow) na uwekaji kumbukumbu unawiana na mifumo ya habari (aligned with information systems),
- ❖ Kanzi data (Data base) zimetengenezwa na zinatumika.
- ❖ Idara, vitengo vijiji na kata vinapata na kutumia mifumo ya habari (accessing and using Information System).
- ❖ Rasilimali zinaelekezwa katika utekekelezaji wa mpango mkakati na taarifa zinatolewa na ufuatiliaji unafanyika.
- ❖ Uwepo wa ofisi bora za idara zenye vitendea kazi na vifaa tosherezi kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa jamii.

**Madhanio/wazo la msingi**

- ❖ TAMISEMI na Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma wameratibu na kuwezesha mabadiliko yote muhimu ya kimuundo na kiutawala
- ❖ Uwepo wa mashirikiano kati ya wafadhiri muhimu (key council donors), jamii na wadau wangine.
- ❖ Sera za serikali zinazo saidia na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri.
- ❖ Uwepo wa ushabihiano na mahusiano ya takwimu kati ya Halmashauri na TAMISEMI.

### 3.4.3 Lengo D: Ubora na idadi ya huduma za kijamii/kiuchumi na miundo mbinu kuongezeka

**Viashiria vya ufanisi**

- ❖ Kiwango cha upelekaji wa fedha kwa ujenzi wa miundo mbinu ya jamii (Social Infrastructure Financing), ushirikishwaji, kiwango cha jamii kupata habari (Reporting Awareness) na ushiriki/utayari wa Asasi za Kiraia (Commitment among CSOs).
- ❖ Uwepo wa upatikanaji na utumiaji wa miundo mbinu ya msingi kwa jamii.
- ❖ Kiwango cha kuzingatiwa kwa taratibu na sheria za mikataba na manunuzi (Compliance in Contracts and Procurement Management) au kutekelezwa/kutimiza malengo utoaji wa huduma za kimiundo mbinu (fulfilling objectives in Social Service Delivery Infrastructure).

**Madhanio/wazo la msingi:**

- ❖ Uwepo wa mashirikiano kati ya wizara ya ardhi & Baraza la usimamizi wa mazingira (NEMC) na Halmashauri ya wilaya ya Missenyi
- ❖ Uwepo wa mashirikiano na wafadhiri na wadau wengine.
- ❖ Uwepo wa mashirikiano na Taasisi ya manunuzi ya umma (PPRA) na TAMISEMI
- ❖ TAMISEMI kuwa na huduma bora zinazounganisha takwimu za Halmashauri zote nchini ikiwemo na Halmashauri ya wilaya ya Missenyi

### 3.4.4 Lengo E: Utawala bora na huduma za kiutawala kuboreshwa.

**Viashiria vya ufanisi:**

- ❖ Sera za ndani ya Halmashauri (Internal policies) na sheria ndogo (bylaw) kuendana na kushahiriana na sera na sheria zilizopo za Taifa/Nchi.
- ❖ Kazi na majukumu vinaendana na kutegemeana na ufanisi (performance), ujuzi/uwezo (skills/competences), mikataba ya OPRAS na mifumo na taratibu za utoaji motisha (Rewards/Motivation Frameworks).
- ❖ Kuzingatiwa kwa viwango vya utoaji huduma vinavyo kubalika (Afya, Elimu, Maji nk water)
- ❖ Agenda za kufatilia utekelezaji wa mpango mkakati inakuwa ni sehemu ya mikutano ya Halmashauri ya robo na mwaka.
- ❖ Malipo, usajiri na malalamiko vinafanywa kielektroniki.
- ❖ Mashitaka na migogoro ndani na nje ya Halmashauri inatatuliwa kwa ufanisi.
- ❖ Kiwango cha ufanisi katika mabaraza ya kata (Ward Tribunals)
- ❖ Tarifa za ukaguzi wa ndani (Coverage of internal audits)

**Madhanio**

- ❖ Uwepo wa chombo/mfumo endelevu wa kusaidia Halmashauri kufanya maboresho ya sheria ndogo na sera za ndani (internal policies).
- ❖ TAMISEMI and Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa umma kusaidia kuweka mfumo wa utendaji kazi kwa weledi (Meritocratic Systems).
- ❖ Uwepo wa rasilimali

- Simu za mkononi na mitandao kuunganishwa na mifumo ya poto (web based portal).
- Utayari na utashi wa kutumia mfumo mpya wa ufuatiliaji na tathimini.

**3.4.5 lengo F:** Ustawi wa jamii, jinsia na uwezeshaji kuboreshwa

**Viashiria vya ufanisi**
- Kiwango cha jamii kitimiza majukumu yao (social obligations).
- Kiwango cha upatikanaji wa haki za msingi kwa jamii (basic social rights)
- Kiwango cha utoaji wa mikopo kwa wanawake na vijana (satisfaction of Loans requests from Women and Youth)
- Kiwango cha malalamiko kutoka kwa wakawake na vijana

**Madhanio**
- Utayari na utashi wa jamii kutimiza majukumu yao kuwa endelevu (social obligations sustained)
- Uwepo wa mazingira bora ya kiuchumi na kijamii (Favorable social –economic environments)
- Uwepo wa uwezo na vipaji vikubwa vya ubunifu miongoni mwa wanawake na vijana viongozi wa vikundi (High creativity and innovation capability)
- Mazingira wezeshi ya kisiasa na kiuongozi (Political and leadership support)

**3.4.6 Lengo G: Maliasili na usimamizi wa mazingira kuboreshwa**

**Viashiria vya ufanisi:**
- Mpango mkakati wa kukusanya na kutupa taka umekubalika, umeigwa na kutekelezwa.
- Kiasi cha taka zilizo kusanywa na kutupwa.
- Uwepo wa mtandao wa kuondoa maji taka (Sewerage connections)
- Kiwango cha uelewa wa jamii juu ya haki na wajibu wao katika matumizi/usimamizi wa ardhi na maliasili.
- Vibali vya ujenzi wa majengo mapya na ukarabati (building/rehabilitation permits)
- Vijiji na kata kusaidia michakato ya utoaji wa vibali.
- Urasimishaji wa maeneo yasiyo rasmi (Informal areas formalized)
- Maeneo yaliyo pimwa kupewa umiliki (New surveyed plots leased out)
- Wasifu wa maeneo ya uwekezaji kutengenezwa na maeneo kumilikishwa na kuendelezwa (Investment Area Profiled and Leased/developed)
- Ekali za mashamba ya miti zinazopandwa kwa mwaka na kuanzishwa kwa akiba za miti za vijiji (Village Forestry Reserves)

**Madhanio/wazo la msingi**

- ❖ Utayari wa jamii kuwekeza katika usimamizi wa taka (waste management) na katika matumizi ya nishati mbadala
- ❖ Uwepo wa chombo cha kuwezesha/saidia utengenezaji wa mkakati wa usimamizi wa taka.
- ❖ Upatikanaji wa rasilima kwa wakati. (Timely availability of Resources)
- ❖ Simu za mkononi na mitandao kuunganishwa na mifumo ya poto (web based portal) wa utoajiwa vibali.
- ❖ Uwepo wa mashirikiano kati ya program ya MKURABITA na wizara ya Ardhi.
- ❖ Soko imara (Market stability)

**3.4.7 lengo H**: Uratibu wa maendeleo ya kiuchumi kuboreshwa

**Viashiria vya ufanisi**

- ❖ Kiwango cha uelewa na matumizi ya mbinu bora za kilimo, uvuvi na mifugo na matumizi ya teknolojia na nyenzo/vifaa bora na upatikanaji wa masoko.
- ❖ Kiwango cha utoaji wa huduma za ugani za kilimo, uvuvi na mifugo Vijijini/Kata.
- ❖ Ujenzi wa miundo mbinu mipya na ukarabati wa iliyopo ikiwemo ile ya machinjio, malambo, maghara, skimu za umwagiliaji, vituo vya kupokelea samaki nk.
- ❖ Idadi za taarifa za pembejeo zisizo kidhi viwango, magonjwa na chamgamoto.
- ❖ Vikundi vya wakulima, wavuvi na wafugaji wanaozingatia sheria na vigezo (complying with laws/standards).

**Madhanio/wazo la msingi**

- ❖ Utayari na utashi wa jamii kubadilika.
- ❖ Upatikanaji wa rasilima kwa wakati.
- ❖ Simu za mkononi na mitandao kuunganishwa na mifumo ya poto (web based portal) na kutumika kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za takwimu na masoko.
- ❖ Uwepo wa utayari wa mashirikiano kati ya wakulima, wafugaji wavuvi na vyama vya usirika.
- ❖ Bei wezeshi ya pembejeo na bei nzuri kwa bidhaa za wakulima, wavuvi na wafugaji.

**3.4.8 lengo I: Udhibiti wa matukio ya majanga na maafa kuboreshwa.**

**Viashiria vya ufanisi:**

- ❖ Uelewa wa jamii na watumishi wa Halmashauri juu ya kudhibiti na kuzuia maafa na majanga.
- ❖ Kupungua kwa mafuriko (Storm water overflows minimized)
- ❖ Kuwekwa/kuanzishwa kwa mkakati wa kutumia mfumo wa Tehama (ICT) kudhibiti majanga na maafa.

**Madhanio/wazo la msingi**

- Utashi endelevu wa jamii kusaidia katika usimamizi wa mifumo ya kutiririsha maji (drainage systems)
- Serikali na wadau wengine kutoa vipaumbele katika usimamizi wa maafa/majanga na kujenga miundo mbinu ya kudhibiti maafa (mitigation infrastructures)
- Uwepo wa mashirikiano kati ya Taasisi ya Serikali Mtandao (e-Government Agency) na TAMISEMI

### 3.4.9 lengo Y: Huduma za lishe za kisekta kuboreshwa (Multi-sectorial nutrition services improved)

**Viashiria vya ufanisi:**

- Kiwango cha utapiamlo miongomi mwa watoto wenye umri kata ya miezi 6 mpaka 56.
- Kiwango cha ufahamu na matumizi ya kiwango cha chini cha mlo kinacho kubalika (Minimum Acceptable Diet “MAD”)
- Kiwango cha unyonyeshaji miongoni mwa wanawake walio jifungua.
- Kiwango cha uelewa na upatikanaji wa virutubisho vya chakula.
- Kiwango cha kiliba tumbo (obesity) miongoni mwa watoto na watu wazima.
- Kiwango cha utapiamulo miongoni mwa watu wazima (elderly persons) na akina mama waja wazito (pregnant women)
- Vituo vya afya (Health facilities) vyenye huduma ya kusimamia utapiamulo mkali (management of Severe Acute Malnutrition)
- Kamati ya uratibu inayoundwa na sekta mbambali (Multi sectoral Coordination Committee) inafuatilia uhamasishaji na uelewa wa jamii wa matumizi ya kiwango cha chini cha mlo kinacho kubalika (acceptable diet sensitization and awareness).

**Madhanio/wazo la msingi**

- Utayari na utashi wa jamii kubadili tabia za ulaji/milo (eating habits/ diets).
- Upatikanaji wa rasilimali kwa wakati.
- Uwepo wa mnyororo imara wa upatikanaji wa chakula (Availability of strong and accessible food supply chain)
- Simu za mkononi na mitandao kuunganishwa na mifumo ya poto (web based portal) kutumika katika kuhamasisha jamii juu ya matumizi ya lishe bora (appropriate diet)
- Uwepo wa mashirikiano na wadau mbalimbali wa sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika kuendeleza upatikanaji wa bidhaa za vyakula vyenye lishe bora kwa bei nafuu

## 4.0. SURA YA NNE

## MFUMO/MUUNDO WA MATOKEO YA MAENDELEO TARAJIWA (RESULT'S FRAMEWORK)

### 4.1. Utangulizi

Mpango Mkakati huu unaweka bayana mfumo/muundo wa namna ambavyo H/Missenyi itaweza kutekeleza malengo yake ya msingi ili matokeo makuu ya maendeleo yanayo kusudiwa/tarajiwa yaweze kutimizwa/kufikiwa. Shabaha kuu ni Halmashauri kutimiza malengo yake ya kuboresha maendeleo ya wananchi ya kiuchumi na kijamii kwa kutumia rasilimali za ndani na nje na kwa kuzingatia misingi ya demokrasia, ushirikishwaji na utawala bora.

Mfumo/muundo (result's framework) utakao tumika unazingatia mahusiano na mifumo mingine ya kitaifa (national frameworks) na unaweka bayana namna ambavyo matokeo tarajiwa ya kila sekta (Afya, Elimu, Kilimo, Maliasili nk) yatashabiriana na matokeo ya sekta nyingine na yatachangia katika kuiwezesha Halmashauri kufikia malengo yake ya maendeleo

Muundo/mfumo unaweka bayana na kounesha namna ambavyo Halmashauri itatumia rasilimali zake za ndani na zile za nje katika kutimiza matokeo yaliyo pangwa (planned outcomes), malengo (objectives), mikakati (strategies), shabaha (targets), shughuli (activities) na nyenzo hitajika (inputs).

Lengo kuu la maendeleo la Halmashuri linawekwa wazi katika na mfumo/muundo wa kimkakati unaokusudiwa kutumika. Aidha mfumo unaweka bayana namna ambavyo malengo mahsusi (specific objectives) yataweza kufikiwa na namna ambavyo matokeo tarajiwa ya maendeleo yataweza kupimwa.

Katika mfumo huu, viashiria mbalimbali vya mafanikio (performance indicator) vilivyo ainishwa vitatumika kupima mafanikio ya malengo na matokeo yaliyopangwa.

Mfumo unaweka bayana mpango ambao Halmashauri utautumia katika kufanya mapitio (review), kufanya ufuatiliaji na kufanya tathimini ya utekelezaji wa malengo na matokeo yaliyo pangwa. Zaidi mfumo unaonesha namna ambavyo utoaji wa taarifa za ndani na nje utafanyika kwa kuweka wazi aina ya taarifa zitakazo tumika, watumiaji/welengwa wa taarifa, muda/vipindi vya kutoa taarifa (mwezi, robo, mwaka nk) na wahusika.

### 4.2. Malengo ya maendeleo

Lengo kuu la Halmashauri ambalo linatoa taswira ya matokeo makuu yanayotarajiwa "kuboresha na kukuza viwango vya maendeleo ya kiuchumi na kijamii vya wanachi wa H/Missenyi". Lengo hili kuu litatekelezwa kupitia malengo mahsusi 8 ambapo kila lengo limewekewa shabaha na mikakati ya kulitekeleza. Wadau mbalimbali watashiriki kikamilifu katika kutekeleza malengo haya. Wadau hawa ni pamija na jamii ya H/Missenyi, Watumishi wa H/Missenyi, Viongozi Wachaguliwa/Kisiasa, Viongozi Waajiriwa, TAMISEMI, Sekretariati Mkoa, Wizara za Kisekta, Wabia/Wafadhiri katika

maendeleo, Mashirika yasiyo ya kiserikari, Taasisi za kidini, Taasisi za uma, Watoa huduma nk.

### 4.3. Mahusiano kati ya mpango mkakati na mifumo/miundo ya kitaifa

H/Missenyi itatoa huduma kwa kuzingatia mifumo/miundo ya kitaifa iliyopo. Mifumo/Miundo hiyo ni pamoja ile ya:

#### 4.3.1 Mfumo/muundo wa kisheri na kisera (Legal & policy framework)

Mfumo/muundo wa kisheria na kisera ni moja ya vitu vya msingi vinavyo hitajika ili wadau mbalimbali waweze kushirikiana na kutimiza wajibu wao katika kutekeleza maendeleo

H/Missenyi itahakikisha uwepo wa weredi katika matumizi ya rasilimali na utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia mifumo/miundo ya taifa ya kisheria na kisera. (National legal and policy framework)

H/Missenyi inakusudia kutoa huduma bora kwa jamii hivyo sheria ndogo zitaundwa na zilizopo zitafanyiwa mapitio ili kuhakikisha kuwa zinashabiriana na kuzingatia mifumo ya kitaifa ya kisheria na kisera.

#### 4.3.2 Mfumo/muundo wa kiutawala (Gorvernance framework)

Ili kutoa huduma bora kwa jamii, H/Missenyi itazingatia misingi ya utawala bora ikiwemo ile ya kuhakikisha kuwa utekelezaji wa shughuli za maendeleo unazingatia muda uliopangwa (right time horizon), unafanywa kwa gharama halisia zinazo lingana na kuendana na ubora wa matokeo yaliyo kusudiwa (value for money) na uwepo wa usawa katika utoaji wa huduma kwa watu wote bila kujali umbali, umri, jinsia, ambali/ukoo (racial) na kipato.

Aidha dhima ya Halmashauri inayo lenga kukuza na kuboresha maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya wananchi wa H/Missenyi kwa kutumia rasilimali zilizopo za ndani na nje na kwa kuzingatia misingi ya demokrasia, ushirikishwaji na utawala bora inaweka wazi mabadiliko hitajika katika utoaji wa huduma na utendaji kazi, usimamizi/matumizi ya rasilimali na inazingatia mfumo/muundo wa kitaifa wa utawala bora. Hivyo mpango mkakati huu ni nyenzo ya kutekeleza mfumo/muundo wa kitaifa wa utawala bora.

#### 4.3.3 Mfumo/muundo wa muda wa kati wa matumizi ya pesa (Medium term expenditure framework)

Maendeleo ni mzunguko unaohusu kutekeleza, kufanya mapitio na tathimini ya utekelezaji na kuainisha mahitaji mapya na hatimaye kuibua mipango inayofuata. Mpango mkakati wa H/Missenyi unahusu upangaji wa mipango kwa mfumo/muundo wa muda wa kati wenye sura/sifa ya upangaji mipango na bajeti ya muda wa kati ambapo makiso ya bajeti yatafanywa kwa kipindi cha miaka mitatu (the forward budget estimate) na kutakuwepo mapitio na tathimini ya utekelezaji na uainishaji wa mahtaji mapya na uibuaji wa mipango mipya inayofuata kila mwaka (annual reviews and reflections)
Mpango mkakati wa H/Missenyi unazingatia mfumo/muundo wa taifa wa muda wa kati wa matumizi ya pesa (MTEF) ambao kimsingi unahusu mchakato wa upangaji mipango ya maendeleo na bajeti kwa njia ya uwazi (transparence) na ushirikishwaji. Mchakato huu unayo malengo makuu mawili; kwanza ni kuweka malengo ya kifedha (fiscal targets)

na pili ni kuelekeza rasilimali kwenye vipaumbele vya kimkakati vilivyo ainishwa kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa.

Ili kuwepo kwa uwajibikaji katika matumizi ya pesa za serikali, H/Missenyi itahakikishi kuwa muundo wa utoaji taarifa za utekelezaji unakwenda sambamba na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa bajeti na matumizi ya pesa kama ilivyo ainishwa katika mpango wa muda wa kati wa matumizi ya pesa.

### 4.3.4 Mfumo/muundo wa uwajibikaji (accountability framework)

Mpango mkakati wa H/Missenyi unahusu ugatuzi wa madaraka na rasilima kwa ngazi za chini za serikali za mitaa (vijiji na kata) sawa na matakwa ya muundo wa kitaifa wa uwajibikaji.

## 4.4 Sura ya mfumo/muundo wa matokeo tarajiwa wa mpango mkakati (Result Framework Matrix)

Mfumo/muundo wa matokeo tarajiwa unaweka bayana malengo ya maendeleo ya H/Missenyi, matokeo kusudiwa yaliyo pangwa na viashiria vya matokeo. Zaidi unaonesha namna ambavyo malengo yatatekelezwa na kutimizwa na namna matokeo yatakavyo pimwa. Viashiria vitatumika kupima maendeleo na ufanisi katika kutekeleza malengo na matokeo yaliyo pangwa.

**Jedwali Na 10. Muundo/Sura ya matokeo tarajiwa**

| Lengo/shabaha kuu ya maendeleo | lengo | Maelezo ya lengo | Matokeo Tarajiwa | Kiashiria cha Kupima Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| H/Missenyi Kukuza kiwango cha kijamii na kiuchumi cha watu wake. | A | Huduma kwa jamii kuboreshwa na maambukizi ya ukimwi kupungua. | Matibabu na Huduma kwa watu waishio na VVU kuboreshwa ifikapo Juni 2025. | Idadi ya wagonjwa/waathirika walio andikishwa/sajiriwa kwa ajili ya kupata dawa za kufubaza virusi (ARVs). |
| | | | Shughuli za kuzuia/kupambana na UKIMWI katika sehemu za kazi kuwezeshwa ifikapo Juni 2025 | Idadi ya idara zilizo tekeleza shughuli za kuzuia/kupambana na UKIMWI katika sehemu za kazi. |
| | | | Kiwango cha maambukizi ya VVU/UKIMWI kupungua kutoka 3% mpaka 1% ifikapo Juni 2025 | Kiwango cha maambukizi ya VVU/UKIMWI. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Huduma za nyumbani kwa watu waishio na VVU kuboreshwa katika kata 20 ifikapo Juni, 2025 | Namba ya waathirika wa VVU walio kubali kwa hiari kujiunga na utaratibu wa huduma kwa waathirika majumbani. |
| | | | Vikundi vya vijana (waliobarehe mpaka miaka 18) vya VVU/UKIMWI nje ya shule kuanzishwa katika kata 20 ifikapo Juni, 2025 | Idadi ya vikundi hai vya vijana vilivyo anzishwa nje ya shule na vinavyo fanya kazi ya kupambana na UKIMWI kwa ufanisi |
| | B | Mkakati wa Taifa wa kupambana na Rushwa Kutekelezwa na kuwa endelevu ifikapo Juni, 2025 | Kuanzishwa utaratibu na kujenga uwezo wa Halmashauri kupokea na kushughulikia malalamiko ya kero zitokanazo na rushwa ifikapo Juni, 2025. | Idadi ya malalamiko yaliyo pokelewa na kufanyiwa kazi. |
| | | | Uhamashishaji na ujengaji wa ufahamu wa jamii juu ya mkakati wa Taifa wa kupambana na Rushwa kufanyika katika kata 20 ifikapo Juni 2025 | Idadi ya kesi za Rushwa zinazo fuata na kukubaliana na sheria na taratibu zilizowekwa. |
| | | | Njia za kuhamasisha na kujenga uelewa wa wanafunzi juu ya madhara ya Rushwa kuanzishwa na kuimarishwa katika kata 20 ifikapo Juni, 2025. | Idadi ya malalamiko ya Rushwa kutoka kwa wanafunzi<br><br>Idadi ya matukio ya kuwahamashisha wanafunzi |
| | C | Upatikanaji wa huduma bora na yenye usawa kuboreshwa | Kiwango cha ufaulu wa darasa la nne na saba kukua kutoka 83.8% mpaka 94% ifikapo Juni, 2025 | Kiwango cha ufaulu katika mitihani ya darasa la nne na saba |
| | | | Kiwango cha uandikizaji wa wafunzi wanaojiunga na darasa la kwanza kuongezeka kutoka 97% mpaka 98% ifikapo Juni, 2025 | Idadi ya wanafunzi walioandikishwa kujiunga na elimu ya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | msingi (darasa la kwanza) |
| | | | Alama ya ufaulu kwa mitihani ya darasa la nne, kidato cha nne na kidato cha sita kuongezeka kutoka 76% mpaka 96% ifikapo Juni 2025 | Alama/Kiwango cha ufaulu katika mitihani. |
| | | | Miundo mbinu katika shule 96 za msingi kuboreshwa kutoka 69% mpaka 80% ifikapo Juni 2025 | Idadi ya shule za msingi zenye miundo mbinu tosherezi |
| | | | Miundo mbinu katika shule za sekondari 22 kuboreshwa kutoka 63% mpaka 78% ifikapo Juni 2025 | Idadi ya shule za sekondari zenye miundo mbinu tosherezi |
| | C | | Kiwango cha vifo vya akina mama/wazazi wakati wa kujifungua kupungua kutoka 0.67 mpaka 0.3 kwa kila watoto 100,000 waliozaliwa hai ifikapo Juni 2025. | Kupungua kwa kiwango cha vifo vya akina mama/wazazi wakati wa kujifungua |
| | | | Kiwango cha vifo vya watoto wachanga wanaozaliwa kupungua kutoka 0.93 mpaka 0.2 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai ifikapo Juni 2025 | Kupungua kwa kiwango cha vifo vya watoto wachanga |
| | | | Zoezi la chanjo ya kuzuia maradhi kuendelea kutolewa kwa kiwango cha zaidi ya 95% ya walengwa kwa chanjo zote ifikapo Juni 2025 | Kiwango cha utoaji wa chanzo za kuzuia maradhi kwa walengwa. |
| | | | Upungufu wa madawa, vifaa tiba na vitendanishi (diagnostic supplies) kupungua kutoka 26% mpaka 10% ifikapo Juni 2025 | Kiwango cha jamii kuridhika/kufurahia huduma za kijamii |
| | | | Viwango vya visa vya malaria kupungua kutoka 8.2% mpaka 4% ifikapo Juni 2025 | Idadi ya wagonjwa walio hudumiwa<br>Mabadiliko katika orodha ya magonjwa kumi yanayoongoza. |
| | | | Upungufu wa miundo mbinu ya afya (Health facility infrastructure) kuboreshwa kutoka 48% mpaka 30% ifikapo Juni 2025 | Kiwango cha jamii kuridhika/kufurahia huduma za kijamii |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Upatikanaji wa huduma za kijamii, afya, mafunzo na huduma ya elimu kwa makundi yaliyo athirika zaidi (most vulnerable groups) kuboreshwa kutoka 45% mpaka 70% ifikapo Juni 2025 | Kiwango cha jamii kuridhika/kufurahia huduma za kijamii |
| | | | Huduma ya maji, unadhifu (hygiene) na usafi wa mazingira kuboreshwa katika kata zote 20 ifikapo Juni 2025 . | Idadi ya kaya zenye uhakika wa kupata maji safi na salama ndani ya umbali wa mita 400 |
| | | | Idadi ya watu wanaopata maji safi na salama kuongezeka kutoka 48% mpaka 73% ifikapo Juni 2025. | Idadi ya kaya zenye uhakika wa kupata maji safi na salama ndani ya umbali wa mita 400 |
| | | | Usafi wa kaya na mashuleni kuongezeka kutoka 54% mpaka 80% ifikapo Juni 2025. | Kiwango cha jamii kuridhika/kufurahia huduma za kijamii |
| | | | Elimu kuboreshwa, kutolewa na kupatikana kwa wote na kwa usawa katika ngazi zote za Chekechea, Msingi na Sekondari ifokapo Juni 2025 | Kiwango cha jamii kuridhika/kufurahia huduma za kijamii |
| | | | Kiwango cha udumavu kupungua kutoka 39% mpaka 20% ifikapo Juni 2025. | Kiwango cha jamii kuridhika/kufurahia huduma za kijamii |
| | | | Ukusanyaji, usafirishaji, uhifadhi na utupaji bora wa taka ngumu kuongezeka kutoka 63% mpaka 80% ifikapo Juni 2025 | Kuongezeaka kwa Ukusanyaji, usafirishaji, uhifadhi na utupaji bora wa taka ngumu |
| | | | Upandaji wa miti rafiki kwa mazingira ipatayo 7,500,000 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la miti rafiki kwa mazingira |
| | D | Ubora na idadi ya huduma za kiuchumi/kijamii na miundombinu kuongezeka | Idadi ya vijiji vyenye maafisa ugani kuongezeka kutoka 30 mpaka 45 ifikapo Juni 2025 | ongezeko la Idadi ya vijiji vyenye maafisa ugani |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi ya maafisa ugani wenye vitendea kazi (extension kits) kuongezeka kutoka 0 mpaka 40 ifikapo Juni 2025 | ongezeko la Idadi ya maafisa ugani wenye vitendea kazi (extension kits) |
| | | | Idadi ya vituo vya rasilimali vya kilimo (WARCs) vilivyo fanyiwa ukarabati na vinavyo fanya kazi kwa ufanisi kuongezeka kutoka 0 mpaka 5 ifikapo Juni 2025 | Idadi ya vituo vya rasilimali vya kilimo (WARCs) vilivyo fanyiwa ukarabati na vinavyo fanya kazi |
| | | | Tija kwa zao la mahindi la kipaumbele katika uwekezaji kuongezeka kutoka tani 2.5 hadi 3.71 kwa hektari ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la tija kwa zao la mahindi |
| | | | Uzalishaji wa zao la mahindi la kipaumbele katika uwekezaji kuongezeka kutoka tani 21,220 hadi 30,300 kwa mwaka ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la uzalishaji wa zao la mahindi |
| | | | Tija kwa zao la kahawa la kimkakati kuongezeka kutoka kilo 3 kwa mti mpaka kilo 5 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la tija kwa zao la kahawa |
| | | | Uzalishaji wa zao la kahawa la kimkakati kuongezeka kutoka tani 910.8 mpaka tani 1,340 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la uzalishaji wa zao la kahawa ifikapo |
| | | | Idadi ya maghara yaliyo jengwa, kufanyiwa ukarabati na kutumika kuongezeka kutoka maghara 4 mpaka 9 ifikapo Juni 2025 | Idadi ya maghara yaliyo jengwa, kufanyiwa ukarabati na kutumika |
| | | | Idadi ya vikundi vya wakulima wanye mashine za kuongeza thamani ya mazao kuongezeka kutoka vikundi 30 mpaka 55 ifikapo Juni 2025 | Idadi ya vikundi vya wakulima wanye mashine za kuongeza thamani |
| | | | Matumizi ya eneo linalo faa kwa kilimo kuongezeka kutoka hektari 64,828.6 mpaka 74,826.6 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la matumizi ya eneo linalo faa kwa kilimo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi ya miundo mbinu ya masoko iliyo jengwa na kufanyiwa ukarabati na inayo tumuka kwa ufanisi kuongezeka kutoka 2 mpaka 7 ifikapo Juni 2025 | Idadi ya miundo mbinu ya masoko iliyo jengwa na kufanyiwa ukarabati na inayo tumuka kwa ufanisi |
| | | | Idadi ya skimu za umwagiliaji iliyo jengwa na kufanyiwa ukarabati na inayo tumuka kwa ufanisi kuongezeka kutoka 0 mpaka 2 ifikapo Juni 2025 | Idadi ya skimu za umwagiliaji iliyo jengwa na kufanyiwa ukarabati na inayo tumuka kwa ufanisi |
| | | | Matumizi ya mbolea za viwandani kuongezeka kutoka tani 114 mpaka 139 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la matumizi ya mbolea za viwandani |
| | | | Vyama vya ushirika kuongezeka kutoka 78 mpaka 83 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la vyama vya ushirika |
| | | | Wakulima wanao anzisha au kujiunga na vyama vya ushirika kuongezeka kutoka 8,176 mpaka 10,676 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la wakulima wanao anzisha au kujiunga na vyama vya ushirika |
| | | | Uzalishaji wa nyama kwa mwaka kuongezeka kutoka tani 517 mpaka 564 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la uzalishaji wa nyama kwa mwaka |
| | | | Uzalishaji wa maziwa kwa mwaka kuongezeka kutoka lita 12,252,626 hadi 14,502,626 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la uzalishaji wa maziwa kwa mwaka |
| | | | Uzalishaji wa mayai kwa mwaka kuongezeka kutoka mayai 3,429,000 hadi 3,754,000 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la uzalishaji wa mayai kwa mwaka |
| | | | Ongezeko la ujenzi na matumizi ya majosho kutoka majosho 18 mpaka 28 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la ujenzi na matumizi ya majosho |
| | | | Ujenzi na matumizi ya mabwawa/malambo kuongezeka kutoka 36 mpaka 46 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la ujenzi na matumizi ya mabwawa/malambo |
| | | | Ujenzi na matumizi ya vibanio kuongezeka kutoka vibanio 13 mpaka 27 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la ujenzi na matumizi ya vibanio |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Huamilishaji kuongezeka kutoka ng'ombe 694 mpaka 1,004 ifikapo Juni 2025. | Ongezeko la huamilishaji |
| | | | Idadi ya ng'ombe walio pigwa chapa kuongezeka kutoka 55,479 mpaka 65,479 ifikapo Juni 2025 | Idadi ya ng'ombe walio pigwa chapa |
| | | | Uzalishaji wa samaki wa kufuga kuongezeka kutoka tani 120 mpaka 195 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la uzalishaji wa samaki wa kufuga |
| | | | Ujenzi na matumizi ya mabwawa ya kufugia samaki kuongezeka kutoka mabwawa 61 mpaka 110 ifikapo Juni 2025 | Ongezeko la ujenzi na matumizi ya mabwawa ya kufugia samaki |
| | | | Idadi ya wafugaji wa samaki kuongezeka kutoka wafugaji 130 mpaka 200 ifikapo Juni 2025. | Idadi ya wafugaji wa samaki |
| | | | Nyenzo/vifaa vya kujifunzia na kufundishia kuboreshwa katika kata 20 ifikapo Juni 2025 | Idadi ya shule zenye nyenzo/vifaa tosherezi |
| | | | Huduma za vituo vya afya 36 (health facilities) kuboreshwa ifikapo Juni, 2025 | Idadi ya vituo vya afya |
| | | | Asilimia ya watu wanaopata maji safi na salama na kumudu gharama kuongezeka kutoka 48% mpaka 73% ifikapo Juni, 2025 | Idadi ya miundo mbinu ya maji inayo toa huduma kwa ufanisi |
| | | | Chuo cha ufundi stadi kimoja kilichopo kuboreshwa na kingine kimoja kuongezwa ifikapo Juni 2025 | Idadi ya vituo vya ufundi vilivyo boreshwa/anzishwa |
| | E | Utawala bora na huduma za kiutawala kuboreka | Uratibu, ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za Halmashauri kuboreka ifikapo Juni 2025 | Kiwango cha wateja kuridhika<br>Kiwango cha uzingatiaj wa sheria na taratibu<br>Idadi ya malalamiko<br>Idadi ya mikutano ya kisheria iliyofanyika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Hali halisi ya taarifa za ukaguzi<br>Kiwango cha kujituma na kuwajibika |
| | | | Usimamizi wa sheria na haki za kisheria za halmashauri kuimarishwa ifikapo Juni 2025 | Kiwango cha uzingatiaj wa sheria na taratibu |
| | | | Kuimarisha ushiriki wa wananchi katika mikutano ya kisheria katika ngazi mbalimbali ifikapo Juni 2025 | Idadi ya mikutano ya kisheria iliyofanyika |
| | | | Ushiriki wa jamii katika kutoa maamuzi kupitia mikutano ya kisheria kuongezeka kutoka 65% mpaka 100% ifikapo Juni 2025 | Kiwango cha wateja kuridhika<br>Kiwango cha uzingatiaj wa sheria na taratibu<br>Idadi ya mikutano ya kisheria iliyofanyika<br>Kiwango cha kujituma na kuwajibika |
| | | | Watumishi wa Halmashauri kujengewa ujuzi hitajika ifikapo Juni 2025 | Idadi ya watumishi waliopata mafunzo rejea (staff retrained ) |
| | | | Ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kuongezeka kutoka Tshs. 1,896,565,290.00 mpaka Tshs. 3,609,708,420.00 ifikapo Juni, 2025 | Ongezeko la mapato ya ndani |
| | | | Mikutano ya kisheria kufanyika kwa kufuata na kuzingatia ratiba ifikapo Juni 2025 | Idadi ya mikutano ya kisheria iliyofanyika kwa kufuata ratiba |
| | F | Ustawi wa jamii, jinsia na uwezeshaji wa jamii kuboreka | Ubora wa maisha kwa waathirika 8670 (most vulnerable) kuboreka ifikapo Juni 2025 | Idadi ya makundi athirika/hatarishi yaliyo tambuliwa<br>Idadi ya vikundi vya kiuchumi vya wanawake na vijana vilivyo wezeshwa |
| | | | Hali ya lishe katika Halmashauri kuboreka ifikapo Juni 2025 | Asilimia ya kupungua kwa utapiamlo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Vikundi vya kiuchumi 71 vya wanawake, 30 vya vijana wenye wasijiweza (disabled) kuwezeshwa ifikapo Juni, 2025 | Idadi ya vikundi vya kiuchumi vya wanawake na vijana |
| | | | Masuala ya kijinsia kuzingatiwa na kuboreshwa katika idara na kata 20 ifikapo Juni 2025 | Kiwango cha uelewa wa jamii wa masuala ya kijinsia |
